



ILEMELA YETU

Jarida la Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela

ROBO YA KWANZA 2022/2023
JULAI- SEPTEMBER 2022
TOLEO Na. 1

HALIUZWI

MAPATO YA NDANI YA HALMASHAURI YALIVYOFANIKISHA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILEMELA

- Tshs. Bilioni 3.41 za mapato ya ndani zatekeleza miradi 50
- Miundombinuu sekta ya Afya na Elimu yaboreshwa
- Wanawake, vijana na watu wenye Ulemavu wawezeshwa



Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela Mhandisi Modest Apolinary akikagua moja kizimba cha Samaki kinachosimamiwa na kikundi cha vijana kilichopewa mkopo wa asilimia 10 ya Vijana na Halmashauri

Ilemela ni yetu, Tushirikiane kuijenga

NENO LA MEYA NA MKURUGENZI



Taifa lolote likisoma ndio maendeleo, tumefanya kazi kubwa katika Sekta ya Elimu yote yamwezekana kwa ushirikiano wa serikali kuu, mapato ya ndani na mbunge wa Jimbo la Ilemela nikiwa kama Mwenyekiti wa Halmashauri kwa kushirikiana na Baraza la Madiwani tunazisimamia hizi fedha.

Hivyo nitoe rai kwa wakazi wote wa Manispaa ya Ilemela kuendelea kushiriki katika washiriki katika shughuli mbalimbali za maendeleo hususan uibuaji wa ujenzi wa miundombinu ya vyumba vya madarasa, zahanati kwa kujenga misingi, Fedha za mfuko wa jimbo zitahusika na kunyanyua boma na ukamilishaji utafanyika na Halmashauri kila mmoja ashiriki katika shughuli za maendeleo kwani serikali ni mimi wewe na yule

Mwisho kabisa nimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutupatia fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa ambapo katika mwaka huu wa fedha 2022/2023 Ilemela imepokea fedha kiasi cha Tshs. Bilioni 2.2 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 110 ikiwa ni maandalizi ya mapokezi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka 2023.

**MHE. RENATUS BAHEBE MULUNGA
MSTAHIKI MEYA WA HALMASHAURI
MANISPAA YA ILEMELA**



Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela imekadiria kukusanya kiasi cha Tshs. Bilioni 68.15 kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato ambavyo ni chanzo cha mapato ya ndani, chanzo cha miradi ya maendeleo hii ikiwa ni mapokezo ya fedha kutoka serikali kuu, wadau wa maendeleo, chanzo cha matumizi ya kawaida, pamoja na chanzo cha mishahara kinachotokana na serikali kuu.

Kwa upande wa chanzo cha mapato ya ndani Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela imekadiria kukusanya kiasi cha Tsh Bilioni 13.52 ambayo ni sawa na asilimia 20 ya bajeti ya Halmashauri, kwa upande wa Miradi ya Maendeleo kiasi cha Tsh Bilioni 10.94 kinakadiriwa kukusanywa kutoka serikali kuu ambayo ni sawa na asilimia 16 ya bajeti, Tshs. Milioni 865.94 kinatarajiwa kupatikana kutoka katika chanzp cha matumizi ya kawaida sawa na asilimia 1 ya bajeti, na chanzo kingine ni mishahara ambayo hulipwa na serikali kuu ambayo ni Tsh Bilioni 42.81 sawa na asilimia 63 ya bajeti yote.

Mapato ya ndani ndio mhimili mkuu katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Halmashauri hususan utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ambapo asilimia 60 ya mapato ya ndani ya Halmashauri hupelekwa katika utekelezaji wa miradi hiyo.

Hivyo ni rai yangu kuwa wote wanaotakiwa kulipa kodi na tozo mbalimbali walipe kwa wakati na bila shuruti ili Manispaa ya Ilemela iweze kutekeleza shughuli mbalimbali na hatimae kuleta maendeleo kwa wana Ilemela na Taifa kwa ujumla.

**ENG. MODEST JOSEPH APOLINARY
MKURUGENZI WA HALMASHAURI
MANISPAA YA ILEMELA**

Yaliyomo

01 Mapato Ya Ndani Ya Halmashauri Yalivyofanikisha Utekelezaji Wa Miradi Ya Maendeleo Ilemela

03 Ujenzi Na Uboreshaji Wa Miundombinu Ya Elimu Ulivyofanikiwa Ilemela

05 Uboreshaji Wa Miundombinu Ya Afya Ilemela Kurahisisha Utoaji Wa Huduma Kwa Jamii

07 Wanawake, Vijana Na Watu Wenye Ulemavu Walivyoweza Kujitegemea Kiuchumi Llemela

09 Fedha Za Tozo Za Miamala Ya Simu Mkombozi Kwa Wanao Kayenze: Wananchi Waishukuru Serikali

11 Kuanza Kwa Stendi Mpya Ya Mabasi Nyamhongolo Wananchi Wapongeza Jitihada Za Serikali

13 Matukio Yaliyojiri Katika Kipindi Cha Julai-Septemba 2022

20 Matukio Katika Picha

21 Utekelezaji Wa Miradi Ya Maendeleo

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILEMELA



*Picha na Habari Na
Violencea Mbakile*

Ukusanyaji wa mapato ni moja ya vipaumbele muhimu vya Serikali ya Awamu ya sita ikiwa na lengo la kujenga uwezo wa ndani wa halmashauri wa kujitegemea kifedha na kupunguza kwa kadri inavyowezekana utegemezi kutoka kwa Wadau wa Maendeleo na kuhakikisha kwamba mipango ya kukuza uchumi na kupunguza umaskini inatekelezwa bila kukwama kwa sababu wa ukosefu wa fedha.

Katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela zoezi la ukusanyaji wa mapato ya ndani limewekewa kipaumbele kikubwa ili kuweza kufanikisha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwa lengo la kuboresha maisha ya wananchi wa Ilemela.

Kwa mujibu wa takwimu katika mwaka wa fedha 2021/2022 Manispaa ya Ilemela ilifanikiwa kukusanya kiasi cha Tshs Bilioni 10.12 sawa na asilimia 105 ya makisio ya bajeti ambayo ilikuwa Tsh Bilioni 9.6 na hivyo kiwango cha ukusanyaji wa mapato kuongezeka kwa asilimia 18 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2022/2021. Na hii ni kutokana na mwitikio chanya wa wananchi wa kulipa kodi, usimamizi makini katika ukusanyaji mapato na kuzibwa kwa mianya ya upotevu ikiwa ni pamoja na ununuzi wa mashine (POS) 103 kwa ajili ya kukusanyia mapato mbalimbali ambapo zilitolewa kwa watendaji wa kata pamoja na mawakala mbalimbali wa Halmashauri

Kupitia ukusanyaji wa mapato ya ndani katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 kiasi cha Tshs. Bilioni 3.41 kimetumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikijumuisha sekta mbalimbali katika Manispaa ya Ilemela ambazo ni sekta za utawala, elimu sekondari na elimu msingi, miundombinu na ujenzi, TEHAMA, ardhi, afya, utoaji wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, pamoja na uboreshaji wa ukusanyaji wa mapato.

Katika sekta ya Elimu kupitia chanzo cha mapato ya ndani kiasi cha Tsh milioni 353.02 zimetumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya elimu msingi ikiwemo ukamilishaji wa ujenzi wa maboma 34 ya vyumba vya madarasa hali iliyopelekea uanzishwaji wa shule mbili mpya za ambazo ni Bujingwa na Buyombe na

kufanya ongezeko la idadi ya shule za msingi kutoka shule 76

mwaka wa fedha 2020/2021 hadi shule 78 mwaka wa fedha 2021/2022.

Aidha kwa upande wa Elimu sekondari kupitia chanzo hicho cha mapato ya ndani kiasi cha Tshs. Milioni 274.54 kimetumika kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu mbalimbali ya shule ikiwemo na ukamilishaji wa maboma 19 ya vyumba vya madarasa na kupelekea ufunguzi wa shule za sekondari mpya 5 ambazo ni Masanza, Semba, Nyamhongolo, Igogwe na Buzuruga na kufanya ongezeko la shule za sekondari kutoka 27 mwaka wa fedha 2020/2021 hadi shule 32 mwaka wa fedha 2021/2022.

Mapato ya ndani ya Halmashauri yameweza kuchangia uboreshaji wa miundombinu katika sekta ya afya ambapo kiasi cha Tshs. 211. 14 kimetumika kwa ajili ya ukamilishaji wa majengo ya mama na mtoto katika zahanati 2 za nyakato, ilemela na uanzishwaji wa jengo wodi ya kina mama katika kituo cha afya cha Buzuruga.

Mafanikio mengine yaliyopatikana kupitia chanzo hiki cha mapato ya ndani ni pamoja na ulipaji wa fidia za ardhi ambapo kiasi cha Tshs. Milioni 732.40 kimetumika, kiasi cha Tshs Milioni 644.58 kimetolewa kama mkopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na walemavu, Tshs. Milioni 102. 17 zilielekezwa katika sekta ya ujenzi na miundombinu, na kwa upande wa sekta ya utawala kiasi cha Tsh Milioni 180.02 kilitolewa na kutumika kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za mtaa pamoja na ununuzi wa magari 4 ili kuwezesha shughuli za ukusanyaji wa mapato na matumizi mengine ya Halmashauri.

Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela imefanikiwa kuongeza wigo wa ukusanyaji mapato kwa kutumia mifumo ya TEHAMA ambapo mapato yameongezeka kutoka Tsh. Bilioni 8.5 Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi Tsh. Bilioni 10.12 Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Ili kuongeza ufanisi na kudhibiti upotevu wa mapato, Manipaa ya Ilemela inatumia mfumo wa kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato katika vyanzo vyote na hatua hii imesaidia kudhibiti upotevu wa mapato. Pamoja na hayo Katika mwaka wa fedha 2021/2022

imefanikiwa kuboresha masoko 7 ambayo yametana wigo wa biashara kwa wananchi. Jumla ya biashara 5835 zimesajiliwa kwenye mfumo na kupewa leseni.

Aidha, Ujenzi wa stendi mpya ya mabasi na maegesho ya malori Nyamhongolo umekamilika na ni matarajio ya Manispaa ya Ilemela kuongeza kiwango cha mapato kutokana na makusanyo ya mradi huo hatua ambayo itapandisha mapato ya ndani kutoka Tsh. Bilioni 10.12 hadi Tsh. Bilioni 13.52 kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Ipo mikakati mbalimbali ambayo Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela imejiwekea ili kuweza kufikia lengo la ukusanyaji wa mapato katika mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo imepanga kukusanya kiasi cha Tshs Bilioni 13.52 kutoka chanzo hicho ikiwemo utoaji wa elimu ya mlipa kodi, ununuzi wa mashine ya kukusanyia mapato pamoja na kuziba mianya yote ya upotevu wa fedha.

Mwaka wa fedha wa 2022/2023 Ilemela inatarajia kutekeleza miradi mbalimbali kupitia chanzo cha hiki cha mapato ya ndani ambapo kiasi cha Tsh Bilioni 7. 38 kinatarajiwa kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo.



YA ELIMU ULIVYOFANIKIWA ILEMELA



*Picha na Habari Na
Violancea Mbakile*

Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela inaendelea kufanya jitihada mbalimbali kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya kujifunzia na kufundishia katika shule zake za serikali za Msingi na Sekondari.

Kupitia serikali Kuu, fedha za mfuko wa jimbo, chanzo cha mapato ya ndani, nguvu za wananchi, wadau mbalimbali pamoja na wananchi, halmashauri ya Manispaa ya Ilemela imeweza kuboresha sekta ya elimu kwa kujenga miundombinu mipya ya madarasa, ofisi za walimu, matundu ya vyoo pamoja na kukamilisha ujenzi wa maboma ya vyumba vya madarasa hatua iliyopelekea uanzishwaji wa shule mpya za msingi na sekondari pamoja na kupunguza uhaba wa madarasa.

Ujenzi wa vyumba hivyo vya madarasa umesaidia kuondoa changamoto mbalimbali za msongamano wa wanafunzi katika madarasa imeboresha ufundishaji na ujifunzaji katika shule, pamoja na kuamsha ari ya kusoma kwa bidii kwa wanafunzi na pia kuongeza bidii ya walimu kufundisha, kuondoa tatizo la kutembea umbali mrefu kwa ajili ya kwenda kupata elimu.

Kwa upande wa Elimu Sekondari kiasi cha Tshs Bilioni Bilioni 2.84 kilipokelewa kutoka serikali kuu ambapo kiasi cha Tshs Bilioni 1.94 ni fedha zilizotolewa kwa ajili ya kukabiliana na ugonjwa wa COVID-19 ambapo Ilemela ilifanikiwa kujenga jumla ya vyumba vya madarasa 97 katika shule zote za Sekondari ambayo yaliwalenga wanafunzi wa kidato cha kwanza kwa mwaka 2022.

Aidha fedha kiasi cha Tsh. Milioni 600 kupitia mradi wa SEQUIP zilipokelewa kwa ajili ujenzi wa shule mpya ya Sekondari katika kata ya Buzuruga ambayo hapo awali haikuwahi kuwa na shule ya sekondari na Kiasi cha Tsh. Milioni 308 kiliidhinishwa na serikali kupitia TASAF kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya Sekondari ya Igogwe.

Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kupitia fedha zake za mapato ya ndani imetumia kiasi cha Tshs. Milioni 274.54 kwa ajili ya uboreshaji wa sekta ya elimu sekondari na kiasi cha Tsh milioni 353.02 kwa ajili ya Sekta ya elimu msingi ambapo kupitia fedha hizo imeweza kukamilisha maboma ya vyumba 34 vya madarasa katika shule za msingi na vyumba 19 vya madarasa katika shule za sekondari, ukamilishaji wa maabara, ujenzi wa matundu ya vyoo, ofisi za walimu, utengenezaji wa viti na meza pamoja na ukamilishaji wa bweni la wasichana katika shule ya Sekondari Bwiru.

Hatua hii ya ufunguzi wa shule hizi mpya za msingi na sekondari zimepelekea kuwa na ongezeko la shule 78 kutoka zilizokuwa 76 na kwa upande wa shule za sekondari ongezeko limekuwa ni shule 32 kutoka shule 27 zilizokuwa kwa mwaka 2020/2021.

Mafanikio mengine ni pamoja na kuongezeka kwa ufaulu ambapo hali ya ufaulu kwa upande wa Elimu Sekondari, imekuwa ikiongezeka na lengo kuu likiwa ni kutokomeza daraja ziro. Ufaulu umeongezeka kutoka asilimia 92 katika mwaka 2020 na mwaka 2021 ufaulu umekuwa asilimia 93 kwa kidato cha nne na kuiwezesha Ilemela kushika nafasi ya 2 kimkoa katika mtihani wa kidato cha nne wa mwaka 2021.

Na kwa upande wa Elimu Msingi kumekuwa na ongezeko la kiwango cha ufaulu wa wanafunzi wa darasa la saba ambapo mwaka 2020 ufaulu ulikuwa asilimia 97.29 na mwaka 2021 ufaulu ulikuwa asilimia 96.5. Aidha, Halmashauri ilishika nafasi ya 2 kimkoa na nafasi ya 7 kitaifa katika mtihani wa darasa la saba wa mwaka 2021.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kupitia chanzo cha mapato ya ndani Inatarajia kutumia kiasi cha Tsh 330 kwa elimu msingi na milioni 340 kwa upande wa elimu sekondari kwa ajili ya uboreshaji wa

miundombinu mbalimbali ya sekta ya Elimu.



KURAHISISHA UTOAJI WA HUDUMA KWA JAMII



Picha na Habari Na Violencea Mbakile

Afya ni rasilimali muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii ambayo Serikali imeiwekea mikakati madhubuti ya kupunguza maradhi na vifo kwa wananchi ili kuongeza umri wa maisha yao. Serikali imekuwa ikitilia mkazo suala la upatikanaji wa huduma bora za afya kwa kila mwananchi hususani kwa wanaoishi katika maeneo ya pembezoni ili kuleta uwiano katika upatikanaji wa huduma hiyo kwa maeneo ya mijini na vijijini.

Huduma za afya nchini zimeendelea kutolewa kwa kiwango cha kuridhisha kutokana na mabadiliko endelevu yanayofanyika katika Sekta ya afya kwa lengo la kuleta uwiano katika upatikanaji wa huduma bora za afya mijini na Cvijijini. Kiasi cha asilimia themanini ya watanzania kufikia miaka ya tisini, tayari wana fursa ya kupatiwa huduma katika umbali wa kilomita kumi.

Serikali imekuwa ikishirikiana na wananchi katika ujenzi wa zahanati, vituo vya afya na hospitali katika

kila kijiji, kata na wilaya kuboresha hali ya maisha

na ustawi wao, kama mojawapo ya malengo ya MKUKUTA na Dira ya Maendeleo 2025.

Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ni miongoni mwa Halmashauri nchini, zinazotekeleza huduma za afya ya msingi kwa mafanikio makubwa kutokana na fedha kutoka serikali kuu, chanzo cha mapato ya ndani pamoja na uhamasishaji na ushirikishwaji wa wananchi

Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni ongezeko la Vituo vya kutolea huduma za Afya ambapo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 Manispaa ya Ilemela imefanikiwa kufungua zahanati mpya 3 ambazo ni Nyamadoke, Lumala na Masemele na kufanya ongezeko la zahanati kutoka 14 na vituo vya afya 3 hadi zahanati 17, vituo vya afya 4 na hospitali 1 ya wilaya ambayo bado ujenzi unaendelea kupitia fedha kutoka serikali kuu.

Katika kuendelea kuboresha huduma ya afya kwa jamii, kwa mwaka wa fedha 2022/2021, Manispaa ya Ilemela kupitia chanzo cha mapato ya ndani kimetumia kiasi cha Tshs. Milioni 211. 141 fedha zilizotumika kwa ajili ya ukamilishaji wa majengo mawili ya kujifungulia katika zahanati za Nyakato na Ilemela, pamoja kuanzisha ujenzi wa wodi ya wakinamama katika kituo cha Afya Buzuruga, mafanikio mengine ni pamoja na ukamilishaji wa nyumba ya watumishi katika kituo cha Afya Sangabuye, uwezeshaji wa shughuli za Afya, pamoja na ujenzi wa jengo la kufulia.

Aidha kiasi cha Tshs. Bilioni 1.45 kilipokelewa kutoka serikali kuu ambapo kati ya fedha hizo kiasi cha Tsh. Mil 500 fedha za zilizotokana na tozo za miamala ya simu zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya kipya cha Kayenze, Milioni 150 zimetumika kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa zahanati tatu (3), na Tshs, Milioni 800 zilipokelewa kwa ajili kuendeleza ujenzi wa hospitali ya wilaya (jengo la upasuaji, wodi 2, mortuary na kichomea taka) katika eneo la Kabusungu

Manispaa ya Ilemela inaendelea kujivunia na mafanikio ya uboreshaji na utoaji wa huduma za afya kwa kuongezeka kwa ukusanyaji wa mapato katika zahanati na vituo vya afya kutokana na kufungwa kwa mfumo wa kielektroniki wa GOTHOMIS katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya hali inayopelekea kuepusha upotevu wa fedha na pia imeondoa urasimu kwa wananchi kwani wagonjwa hulipia matibabu kwa mfumo wa kielektroniki.

Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ina vituo 17 vya kutolea huduma za afya vinavyomilikiwa na Serikali ambapo vipo vituo 4 vya afya na zahanati 17, Taasisi 05, Mashirika ya Kidini 3 na watu binafsi 28. Pamoja na huduma nyingine vituo hivi hutoa huduma za wagonjwa wa nje (OPD), uzazi na watoto, ushauri nasaha na kupima (CTC) na kutoa huduma za afya mashuleni

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 kiasi cha Tshs, Milioni 916.28 kinatarajiwa kutumika kutoka katika chanzo cha mapato ya ndani ya Halmashauri katika sekta ya afya kwa ajili ya ukamilishaji wa miundombinu ya zahanati mpya katika mitaa ya Bezi, Ibungilo na Kabangaja, ujenzi wa kituo cha afya kipya, manunuzi



am:



Wanavyowezechwa Kujitegemea Kiuchumi Ilemela



*Picha na Habari Na
Violencea Mbakile*

Kila Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania, zinao wajibu wa kutenga asilimia kumi ya mapato yanayokusanywa kutoka kwenye vyanzo vya ndani vya mapato kwa ajili ya kutoa mikopo kwa vikundi vilivyosajiliwa vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu hii ni kwa mujibu wa kanuni 4.-(1) ya Kanuni Za Utoaji Na Usimamizi wa Mikopo Kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana Na Watu Wenye Ulemavu.

Awali fedha hizo za mkopo kwa makundi hayo mawili zilikuwa zikitolewa kwa masharti ya riba, ya asilimia 10 kwa mwaka na kufikia mwaka 2017 serikali iliziagiza mamlaka za serikali za mitaa kuongeza kundi la walemavu.

Pamoja na hayo ili kuweza kuwasaidia Wanawake, vijana na walemavu kujikwamua kiuchumi, mwaka 2018 serikali iliamua kuwa mikopo hiyo itolewe bila riba ili kuwapa fursa wanawake, vijana na walemavu kwa ajili ya kuanzisha miradi kwa wingi ya kujikwamua kiuchumi kwani suala la riba limekuwa kikwazo kwa makundi mengi kuweza kukopa na kurejesha mikopo kwa wakati.

Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kama ilivyo Halmashauri zingine nchini ili kuhakikisha hilo linafanikiwa imeendelea kutekeleza agizo hilo kwa kutenga asilimia 10 kutoka katika vyanzo vya mapato ya ndani pamoja na kutoa mikopo hiyo kwa wanawake, vijana na walemavu. Ambapo asilimia 4 ya mapato ya ndani huelekezwa kwa wanawake, asilimia 4 kwa ajili ya vijana na asilimia 2 hupewa watu wenye ulemavu.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 Tsh Milioni 644. 58 zilitolewa kwa vikundi 102 ambapo kati ya vikundi hivyo vikundi 76 ni vya wanawake, vikundi 21 ni vya vijana na vikundi 5 ni vya watu wenye ulemavu ikiwa ni ongezeko la asilimia 29 ukilinganisha na kiasi cha Tshs milioni 501 zilizotolewa katika kipindi cha mwaka 2022/2021.

Kupitia mikopo hii isiyokuwa na riba vikundi hivi vimeweza kujikwamua kiuchumi kufuatia shughuli mbalimbali ambazo hujishughulisha nazo kama vile biashara ndogondogo, utengenezaji wa batiki, sabuni

za maji, kilimo cha bustani., biashara ya dagaa na samaki ufugaji wa kuku,pamoja ufugaji wa samaki kwa njia za vizimba .

Vikundi vya catfish na chapakazi ni moja ya vikundi vya vijana ambavyo ni wa nufaika wa mkopo wa vijana kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ambapo katika mwaka wa fedha 2021/2022 vilipata mkopo kiasi cha Tshs milioni 91 na kuwawezesha kuanzisha mradi wa ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba wakiwa na matarajio ya kuvuna tani 32 ya samaki ikikadiriwa kuwa na thamani ya Tshs. Milioni 160 kutoka katika kila kizimba kimoja cha samaki

Baragi Kitabara ambae ni Mwenyekiti wa kikundi cha catfish ameushukuru uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kwa kupewa kipaumbele na kuwawezesha kutekeleza mradi huo wa vizimba huku akishauri kuwa mkopo huu usiishie kwao tu bali uendelee kusaidia na vijana wengine kwa kuwa kuna uhitaji wa vijana wengi katika upatikanaji wa mitaji.

Aidha amewashauri vijana wanaotarajia kupata mkopo huu kuhakikisha kuwa wanakuwa na wazo la mradi tarajiwa na kufanyia utafiti kabla ya kuomba mkopo huo kwani bila kufanya hivyo wataishia kugawana fedha hizo huku akiwataka kuwa wavumilivu kwa kutokutaka kufanikiwa kwa haraka kwani hakuna maisha ya haraka.

“Niwashauri vijana wenzangu kabla ya kuomba mkopo wahakikishe wana wazo la mradi na kulifanyia utafiti kwani kama huna wazo la mradi hamna kitakachofanyika zaidi ya kuishia kugawana na kuishia mitini”, ameshauri ndugu Baragi

Kikundi kingine kilichonufaika na mkopo huu ni kikundi cha wanawake kinachojulikana kwa jina “Ebenezer Women Group” ambacho kinajishughulisha na mashine ya kusaga, pia kinalo duka la rejareja ambapo kiasi cha asilimia ya mauzo yao hutumika kwa ajili ya kuleta tabasamu kwa watoto yatima Kikundi hiki kilipatiwa kiasi cha Tshs. Milioni 37 ikiwa ni asilimia 4 ya mapato ya ndani ya Halmashauri.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikan kupitia mikopo hii zipo changamoto mbalimbali ambazo

Halmashauri imekuwa zikikabiliana nazo katika suala hili la utoaji wa mikopo ambazo ni pamoja na baadhi ya vikundi kutokurejesha mkopo kwa wakati, vikundi vingi vya vijana vinavyopata mkopo huu husambaratika hivyo kupelekea kutokurejesha mkopo.

Kwa upande wa vikundi vya walemavu wamekuwa wakidhani mkopo huu ni ruzuku hivyo hawarejeshi kabisa au hurejesha kwa kusuasua hivyo.Vikundi vingine hubadili matumizi ya mikopo tofautio na miradi waliyoombea hivyo kupelekea kutofikia malengo yaliyotarajiwa.

Ili kuweza kukabiliana na changamoto hizo, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela imejiweka mikakati mbali ya kuhakikisha kuwa fedha hizi zinaendelea kuwanufaisha makundi haya na kuweza kujikwamua kiuchumi baadhi ya mikakati hiyo ikiwemo ni ufuatiliaji wa marejesho ambapo ipo timu maalum ya ufuatiliaji inayohusisha wataalam wa maendeleo pamoja na madiwani wa viti maalum ikiwa ni pamoja na kuendelea kuwapa elimu ya namna ya kuandika maandiko mradi pamoja na elimu ya urejeshaji wa mikopo .

Ipo mikakati mbalimbali ambayo imewekwa katika kuhakikisha kuwa makundi haya yanawezeshwa na kujikwamua na suala zima la umaskini ikiwemo kuhakikisha kuwa makundi haya yanapewa mkopo mkubwa katika kila kata ambao utawawezesha kutekeleza mradi mkubwa ambao utakuwa wa mfano kwa jamii, pia kuendelea kutoa mikopo midogo midogo kwa makundi hayo.

Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela inatarajia kuchangia kiasi cha Tsh. Biloni 1.2 ambayo itatokana na asilimia 10 ya makusanyo ya ndani katika mwaka wa fedha 2022/2023.





Picha na Habari Na Violencea Mbakile

Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela imepokea fedha kiasi cha Shilingi Milioni mia tano, fedha iliyotokana na tozo za miamala ya simu kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya ambacho kimejengwa katika kata ya kayenze hivyo kujulikana kama kituo cha afya kayenze

Ujenzi wa kituo hiki cha afya cha Kayenze ulianza rasmi mwezi wa kumi mwaka 2021 ambapo zoezi la kuchimba msingi liliongozwa na Mkuu wa wilaya ya Ilemela Mhe Hasan Masala kwa kushirikiana na wananchi wa kata hiyo ya Kayenze na kujengwa majengo mawili ya awali ambayo ni jengo la wagonjwa wa nje (OPD), jengo la maabara na kichomea taka.

Kukamilika na kuanza kutumika kwa kituo cha afya Kayenze kunatarajia kuondoa changamoto mbalimbali za wananchi wa kata hiyo hususan kutembea umbali mrefu kwenda kutafuta huduma za afya, kupunguza vifo vya wajawazito na watoto, kuondoa msongamano katika kituo cha afya cha jirani cha Sangabuye pamoja na uboreshaji wa huduma za afya katika Manispaa ya Ilemela.

Haya yamethibitishwa na wananchi mbalimbali wa kata hiyo.

Issa Mwalukila ambae ni diwani wa kata ya Kayenze alikuwa na haya ya kusema, "Kituo hiki cha afya Kayenze kilikuwa ni hitaji kubwa la wananchi wa kayenze, ili kuweza kupata huduma. Wananchi wamepokea na wameshiriki kila kazi zilizokuwa zikiendelea katika ujenzi huu ombi letu kubwa kwa sasa ni kuiomba serikali kujenga wodi za wagonjwa, wakina mama wajawazito na jengo la kuhifadhia maiti kwani huduma ya kuhifadhi maiti wanaipata kituo cha afya karume ambapo ni mbali na gharama ya kusafirisha mwili wa marehemu ni kubwa"

Hamza Bakari, mwananchi wa Kata ya Kayenze amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwaletea tozo ambazo zimefanikisha ujenzi wa kituo hiki kwani changamoto waliyokuwa nayo ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma ya afya katika kituo cha afya Karume ilikuwa ni kubwa sana huku akiwaomba watumishi wa afya kuhakikisha wanatoa huduma sahihi kwa wananchi.

Doto Dede mkazi wa kata ya Kayenze alikuwa na haya ya kusema; "Kihistoria mji wa kayenze umeanza muda mrefu na haujawahi kuwa na kituo cha afya kama hiki na hivyo kuwapelekea wananchi kusafiri umbali mrefu wa takriban kilomita 20 kwenda na kurudi hivyo kuleta adha kwa watu wenye umri mkubwa, watoto na wakina mama wajawazito, ilikuwa shida pamoja na changamoto ya gharama ya nauli ya kuwafikisha katika kituo cha afya sangabuye. Mradi huu umewagusa wananchi moja kwa moja kwani una tija sana kwa wananchi wa kipato cha chini"

"Kituo hiki cha afya kinaenda kuwa mkombozi kwa wananchi wa kata hii kwani awali hawakuwa na huduma zozote za afya, uhitaji bado ni mkubwa kwani wingi wa watu ni kubwa katika jamii hii, hivyo wananchi wanatakiwa kuelewa kuwa fedha hizi za tozo za miamala ya simu zina faida kubwa kwa jamii kwa kizazi kilichopo na kizazi kinachokuja kwasababu faida ya afya kila mmoja anaifahamu".Haya yalisemwa na mmoja wa wananchi wa kata hiyo ya Kayenze

Samson Marwa ambae ni mganga Mkuu katika Manispaa ya Ilemela nae alipata fursa ya kueleza hisia zake na kusema kuwa,"Ongezeko la kituo hiki kwake ni faraja kwasababu itaendelea kupunguza vifo vya wakinamama wajawazito na watoto,ambalo bado ni changamoto nchi nzima huku akitoa ombi maalum kuongezewa majengo mengine ikiwa ni pamoja na ujenzi wa nyumba za watumishi".

Aidha aliongeza kusema kuwa, Ujenzi wa Kituo hiki cha afya kinafanya idadi ya vituo vya afya katika Manispaa ya Ilemela kuongezeka kutoka vituo vitatu hadi vinne ambapo huduma mbalimba zitatolewa kama vile uzalishaji, vipimo vya amagonjwa yasiyoambukiza, vipimo vya magonjwa ya haraka (rapid test), huduma za mama na mtoto pamoja na utoaji wa ushauri nasaha.

Hadi sasa jumla ya majengo sita yamejengwa ambayo ni Jengo la wagonjwa nje, Jengo la maabara, wodi ya wazazi, jengo la upasuaji, jengo la kufulia, na kichomea taka.Kituo cha afya Kayenze kinatarajia kuhudumia kaya takriban 3000.



WANANCHI WAPONGEZA JITIHAHA ZA SERIKALI



*Picha na Habari Na
Violencea Mbakile*

Wananchi mbalimbali wamepongeza jitihada za Serikali chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa hatua ya ukamilishaji wa stendi mpya ya Mabasi na maegesho ya malori Nyamhongolo

Katika nyakati tofauti wananchi waliofika katika stendi hii mpya kwa ajili ya kupata huduma ya usafiri wamepongeza kwa kusema kuwa ni stendi ya kisasa yenye mandhari nzuri ya kuvutia, eneo kubwa la kupumzikia wasafiri pamoja na kupaki magari tofauti na ilivyokuwa stand ya zamani ya mabasi ya Buzuruga, huku wakiiomba Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kuzitatua changamoto ndogondogo ili kuweza kukidhi mahitaji ya wasafiri

Nao wafanyabiashara waliopo katika stendi ya Nyamhongolo wakiwemo wamepokea kwa furaha kuanza kutumika kwa stendi hii kwani kwao ni fursa kubwa kibiashara kwani kutawaongezea wateja huku wakishauri ikiwezekana iwe ni Stendi ya Mkoa ili kuwaongezea kipato chao huku wakihimiza ustaarabu katika matumizi ya stendi hii kudumishwa na kuahidi ushirikiano kwa Manispaa ya Ilemela. Mhandisi Modest Apolinary, Mkurugenzi wa

Manispaa ya Ilemela amemshukuru Mhe. Rais Samia Suluhu kwa kutoa kipaumbele kwa Ilemela na kutoa fedha zilizofanikisha ukamilishaji wa stendi hii kubwa na ya kisasa huku akiwakaribisha wananchi kutumia fursa ya uwepo wa stendi hii kufanya biashara ili kuweza kuinua uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla

Tunakadiria kukusanya takribani kiasi cha Shilingi Bilioni Moja kwa mwaka na hivyo kuchangia ongezeko la mapato ya ndani ya Halmashauri ambapo katika mwaka wa fedha 2022/2023 Ilemela imekadiria kukusanya kiasi cha Tshs. Bilioni 13 kutoka katika chanzo cha mapato ya ndani.

Stendi hii ambayo ilianza kujengwa mwaka 2019 na kukamilika mwezi wa nne mwaka 2022 imegharimu kiasi cha shilingi Bilioni 26.6 za kitanzania fedha kutoka Serikali kuu ikiwa imegawanyika katika maeneo mbalimbali ikiwemo eneo la kuegesha malori takribani 80, eneo la stendi ya mabasi yenye uwezo wa kubeba mabasi 120, jengo la hoteli lenye vyumba 100, eneo la gereji, eneo la godown lenye uwezo wa kuchukua tani 5400, pamoja na maduka takriban 146.

MAJENGO MBALIMBALI KATIKA STENDI YA MABASI NA MAEGESHO YA MALORI



MWEZI JULAI

MWENGE WA UHURU WAPITIA MIRADI 7 YA GHARAMA YA TSHS. BILIONI 1.9

UKAMILISHAJI WA UJENZI WA BWENI JIPIYA LA WAVULANA SHULE YA SEKONDARI BWIRU



Mwenge wa Uhuru ulipokelewa Wilaya ya Ilemela mnamo tarehe 15 Julai 2022 ukitokea Wilaya ya Magu

Mnamo tarehe 29/06/2022, majira ya saa tatu usiku Bweni la Lumumba katika shule ya sekondari ya wavulana ya Bwiru, liliteteketwa na moto (chanzo hakijajulikana),

Ukiwa Wilaya ya Ilemela ulikimbizwa Km 84.1 ambapo ulipitia miradi 7 yenye gharama ya Tshs Bilioni 1.9 katika ya miradi hiyo, Miradi miwili iliwekwa mawe ya msingi, miradi 5 ilizinduliwa na Jumla ya shughuli 5 zilikaguliwa.

Kwa mujibu Mkuu wa Shule hiyo Mwalimu Thomas Werema alisema moto umeteketwa vifaa vyote vilivyokuwemo kwenye bweni hilo wakati wanafunzi wakiwa darasani wanajisomea na waliopata majanga ni wanafunzi 76 wa kidato cha kwanza na lakini wote wapo salama hakuna aliyedhurika.

Miradi iliyowekwa mawe ya msingi ni Majengo matatu katika kituo cha afya Kayenze, na Barabara ya Breweries, Miradi iliyozinduliwa ilikuwa ni Mradi wa Vijana wa ufugaji samaki kwa njia ya Vizimba, anwani za makazi, ujenzi wa vyumba vine vya madarasa katika shule ya Sekondari Bujingwa vikivyojengwa kwa fedha za UVIKO-19, Mradi wa Mtu Binafsi (Kituo cha Mafuta ASHICO), na mradi wa maji mlima Rada

Kufikia tarehe 19 mwezi wa saba ujenzi wa bweni jipya kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza lilikamilika kwa gharama ya Tshs. Milioni 71.81 kutoka katika mapato ya ndani ya Halmashauri iliyojumuisha manunuzi ya vitanda na magodoro. Pamoja na hayo wadau mbalimbali ambao ni NMB, DESK AND CHAIR FOUNDATION, CRDB waliwashika mkono wanafunzi hao kwa kutoa vifaa mbalimbali.

Mwenge wa Uhuru ulikimbizwa ukienza Kauli mbiu juu ya masuala ya Sensa isemayo, "Sensa ni Msingi wa mipango ya maendeleo, shiriki kuhesabiwa tuyafikie malengo ya Taifa", na ulikabidhiwa Wilaya ya Ukerewe siku ya Tarehe 16 Julai 2022

Bweni hili jipya linao uwezo wa kulaza wanafunzi 80 ukilinganisha na la awali lililokuwa na uwezo wa kulaza wanafunzi 76.



MWEZI AGOSTI

HAFLA YA UGAWAJI WA MADAWATI KWA SHULE ZA MSINGI ILEMELA



Mnamo tarehe 26 Julai Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Mhe. Hassan Masala alikabidhi madawati madawati 431 kwa shule 21 ikiwa ni awamu ya kwanza lengo kubwa ikiwa ni kupunguza changamoto za kujifunza na kujifunzia, kwa wanafunzi wa shule za msingi ilemela.

Upatikanaji wa madawati haya ni matokeo ya harambee iliyoratibiwa nae siku ya tarehe 31 Mei 2022 ambapo lengo ilikuwa ni kupata madawati 1000, lakini lengo lilivuka na hivyo kupatikana madawati 1500 kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo.

Katika Harambee hii Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ilichangia kiasi cha Tshs. Milioni 35 sawa na madawati 500 ambapo wadau mbalimbali walichangia takribani kiasi cha Tshs Milioni 72 na wadau wengine waliwasilisha madawati.

RC MALIMA AJITAMBULISHA RASMI ILEMELA TAREHE 04 AGOSTI 2022



Tarehe 4 Agosti 2022, Mhe. Adam Kighoma Malima, aliwasili Ilemela kwa lengo la kujitambulisha rasmi mara baada ya kuteuliwa kuongoza mkoa wa Mwanza ambapo alipata

fursa ya kuongea na watumishi wa Ilemela na

kutoa maelekezo mbalimbali kubwa zaidi ni suala la ukusanyaji wa mapato.

Alihitimisha ziara yake kwa kukagua stendi ya mabasi ya Nyamhongolo ambapo aliridhishwa na ujenzi huo pamoja na ubunifu uliofanyika katika stendi hiyo.

UZINDUZI WA MAJENGO YA MAMA NA MTOTO



Tarehe 06 Agosti 2022, Mhe. Dkt. Angeline Mabula Munge wa Jimbo la Ilemela na Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi alizindua majengo mawili ya mama na mtoto katika Zahanati za Ilemela na Nyakato pamoja na kuweka jiwe la msingi katika kituo cha Afya Buzuruga kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya kinamama.

Mhandisi Modest Apolinary Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela akisoma taarifa ya miradi hiyo alisema kuwa kupitia chanzo cha mapato ya ndani Manispaa ya Ilemela imetoa takriban kiasi cha Tsh. Milioni 72. 4 kwa ajili ya kukamilisha majengo mawili ya mama na mtoto katika zahanati za Ilemela na Nyakato ambazo zilikuwa zimekaa kwa muda mrefu bila kukamilika huku kiasi cha Tsh. Milioni 50 kimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa jengo jipya la Wodi ya wazazi katika kituo cha Afya Buzuruga .

ILEMELA YAIBUKA MSHINDI WA PILI MAONYESHO YA NANENANE 2022

Kila tarehe nane ya mwezi wa nane Tanzania Kihudhimisha sikukuu ya wakulima ambapo na Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela imekuwa ikishiriki maonyesho hayo.

MWEZI AGOSTI

Mwaka 2022 Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ilishika nafasi ya pili kati ya Halmashauri 12 zilizoshirika kwa upande wa kanda ya ziwa magharibi

Maonyesho hayo yaliyoanza tarehe 01 mwezi wa nane na kuhitimishwa tarehe nane mwezi wa nane yaliambatana na kauli mbiu isemayo: Agenda 10/30: Kilimo ni Biashara, shiriki kuhesabiwa kwa mipango bora ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi



STENDI MPYA YA MABASI NYAMHONGOLO YAANZA KUTUMIKA RASMI



Stendi mpya ya mabasi Nyamhongolo yenye uwezo wa kubeba mabasi zaidi ya 100 kwa wakati mmoja imeanza kufanya kazi siku ya leo tarehe 16 Agosti 2022 mara baada ya kukamilika kwa ujenzi wake.

Abiria mbalimbali waliofika katika stendi hii kwa ajili ya kupata huduma ya usafirishaji wamepongeza serikali kwa kukamilika kwa stendi hii ya kisasa na kuiomba Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kutatua changamoto ndogondogo ili kuweza kukidhi mahitaji ya wasafiri.

Takriban Tsh.Bilioni 1.7 zinatarajiwa kukusanywa kwa mwaka huu wa fedha 2022/2023 itakayotokana na mapato mbalimbali ya stendi, amesema Mkurugenzi Wa Manispaa ya Ilemela Mhandisi Modest Apolinary.



WATENDAJI WA KATA ILEMELA WAPATIWA VITABU 160 VYA REJISTA ZA WAKULIMA



Vitabu 160 vya rejista za wakulima kwa ajili ya ruzuku ya mbolea vilitolewa kwa watendaji wa kata 19 za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kwa lengo la kupata takwimu sahihi na halisi za wakulima ili kuwezesha kusajiliwa katika mfumo rasmi kwa ajili ya kuja kupatiwa ruzuku ya mbolea hapo baadae.

Afisa Kilimo wa Manispaa ya Ilemela Bi.Neema Semwaiko akiwakabidhi vitabu hivyo amewataka watendaji wa kata kuwa makini katika zoezi la usajili wa wakulima wote waliopo ndani ya maeneo yao ili kurahisisha zoezi la ugawaji wa mbolea.

Aidha Bi.Semwaiko amewasisitiza kuwa kila mkulima ataandikishwa mahali shamba lake lilipo hata kama wamiliki wa shamba ni zaidi ya mmoja atasajiliwa mtu mmoja tu kwa niaba ya wengine lengo likiwa kurahisisha zoezi la ugawaji punde taratibu zote zitakapokamilika.

Mpango huu wa ruzuku ya mbolea kwa wakulima unasimamiwa na mamlaka ya udhibiti wa mbolea Tanzania (TFRA) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika mnyororo wa thamani wa mbolea ikiwemo tawala za mikoa na serikali za mitaa (TAMISEMI), serikali za mitaa, mabenki ya biashara na wafanyabiashara wa mbolea nchini.



NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI MHE. ABDLLAH ULEGA ATEMBELEA MRADI WA VIJANA



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Abdallah Ulega amesema kuwa uchumi wa bluu ni fursa kubwa na yenye kuwezekana kutokana na uhitaji mkubwa wa mazao ya samaki nchini na nje ya nchi.

Aliyasema hayo alipotembelea mradi wa vijana wa ufugaji samaki kwa njia ya vizimba uliopo Kata ya Sangabuye eneo la Igalagala ambapo amewapongeza vijana hao kwa hatua hiyo waliyofikia na kuwataka waombe mkopo ili waweze kuwa na vizimba hata 30 kuwawezesha kupata samaki wengi zaidi, pesa nyingi zaidi ili waweze kuajiri na vijana wengine. Kwani kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Wizara takriban vizimba 600 vinawezekana kuwekwa katika eneo la ziwa Viktoria.

Aidha alisema kuwa Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan ameweka fedha jumla ya Tsh. Bilioni 20 katika benki ya kilimo kwa ajili ya kuweza kuinua makundi ya vijana, wakinamama na watanzania wote wenye kutaka kufanya kazi ya uzalishaji mali ili kulijenga taifa la Tanzania kupitia fursa ya uchumi wa bluu. Huku akiwasisitiza vijana ambao tayari wameianza hii kazi na wanaotarajiwa kuanza na walio na utayari, fedha hizi zipo tayari ziingie katika uzalishaji.

Pamoja na hayo aliupongeza Uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Ilemela kwa uthubutu na kuweza kutoa takriban milioni 90 na kuzipeleka katika sekta ya uzalishaji ili kuweza kuwainua vijana hawa wa kitanzania.

ZOEZI LA SENA YA WATU NA MAKAZI ILEMELA LAFIKIA LENGU



Utekelezaji wa zoezi la sensa ya watu na makazi ulianza tarehe 21 Agosti 2022 kwa makarani pamoja na wasimamizi kukutana na viongozi wa Serekali za Mitaa, kukagua mipaka ya maeneo yao, kutambua huduma za jamii na kisha kujaza dodoso la jamii.

Aidha usiku wa sensa (22 Agosti kuamkia 23 agosti 2022) makarani walifika katika maeneo ya kuhesabia watu na kuanza rasmi zoezi la sensa kwa kujaza dodoso la makundi maalumu.

Zoezi la kuhesabu watu kupitia dodoso kuu la sensa liliendelea kuanzia tarehe 23 hadi 29 Agosti, katika kipindi hiki, makarani walipita kila kaya wakiongozwa na viongozi wa maeneo husika kwa ajili ya kudodosa na kujaza taarifa za kidemografia, kiuchumi na kijamii kwa watu waliolala katika kaya husika usiku wa kuamkia tarehe 23 Agosti 2022.

Aidha, zoezi la sensa ya watu na makazi lilihitimishwa kwa makarani kujaza dodoso la majengo kuanzia tarehe 30 Agosti hadi 01 Septemba 2022 ambapo makarani kwa kushirikana na viongozi walipita katika maeneo yao na kujaza dodoso la majengo kwa kuzingatia idadi ya viwanja, majengo/ nyumba na uniti zilizopo katika maeneo hayo pamoja na kuainisha matumizi yake.

Kufanikiwa kukusanya taarifa za sensa ya watu na makazi katika kaya 126,179 kati ya kaya 121, 542 sawa na asilimia 104 ya lengo tarajiwa Kufanikiwa kuhesabu jumla ya majengo 95,418 kutoka maeneo yote ya kuhesabia watu Wilaya ya Ilemela Kufanikiwa kukamilisha zoezi la sensa ya watu na makazi ndani ya muda uliopangwa.

BARAZA LA MADIWANI LAPITISHA TAARIFA YA UTEKELEZAJI YA MWAKA 2021/2022

Mnamo tarehe 26 mwezi Agosti mwaka 2022 ulifanyika mkutano wa mwaka ambapo mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela aliwasilisha taarifa ya utekelezaji katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022

MWEZI SEPTEMBER



Zoezi la utoaji wa chanjo ya polio awamu ya tatu kwa watoto chini ya miaka mitano (5) lilifanyika kwa siku 3 kuanzia tarehe 01 hadi 04 Septemba 2022 na lengo ilikuwa ni kutoa chanjo hiyo kwa watoto 111, 474

Hadi zoezi linakamilika jumla ya watoto 131928 walichanjwa kati yao wakiume walikuwa 52773 na wakike walikuwa 79155 na hivyo kuvuka lengo la asilimia 100 hadi kufikia asilimia 118.

Ugonjwa wa POLIO ni hatari kwani unaweza kusababisha mgonjwa kupooza na hatimae kifo. Watoto chini ya miaka mitano wapo katika hatari kubwa ya kupata ugonjwa huu kwani unapatikana kwa kutozingatia kanuni za usafi na endapo mtoto mmoja atakuwa tayari ana ugonjwa anaweza kuambukiza wengine wengi kwa haraka. Kauli mbiu ya utoaji chanjo ilikuwa ni "mpe matone, okoa maisha"



UTEKELEZAJI WA MFUMO MPYA WA MIKOPO YA 10% YA HALMASHAURI (TPBM)



Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ilianza rasmi kutumia mfumo wa kielekitroniki wa utoaji mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani mnamo tarehe 07 septemba 2022 kwa kutoa mafunzo kwa wataalam wa maendeleo ya jamii na wataalam husika wa mfumo huo.

Mkutano wa Mwaka wa Halmashauri hufanyika kila baada ya mwaka wa fedha kukamilika kwa ajili ya uwasilishaji wa utekelezaji wa shughuli mbalimbali katika Halmashauri, mafanikio yaliyopatikana pamoja na matarajio ya mwaka wa fedha mpya

Mhandisi Modest apolinary alisema kuwa katika kipindi cha mwaka 2021/2022 Halmashauri ilipokea fedha kiasi cha Tshs. Bilioni 34.01 kutoka katika vyanzo mbalimbali na kutumia kiasi cha Tshs. Bilioni 32.37.

Kwa mujibu wa kanuni za kudumu za Halmashauri hufanyika uchaguzi wa naibu meya, uundaji wa kamati za kudumu pamoja na uwasilishaji wa taarifa ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za halmashauri

Baraza hili lilimchagua na kumpitisha Naibu Meya Mhe. Manusura Lusigaliye diwani wa kata ya Buzuruga ambae ataongoza kipindi cha awamu ya pili kwa mwaka 2022/2023 pamoja na kuunda kamati za Kudumu za Halmashauri.



CHANJO YA POLIO AWAMU YA TATU: WATOTO 131,928 WACHANJWA



MATUKIO YALIYOJIRI KIPINDI CHA MWEZI JULAI HADI SEPTEMBER 2022/2023

Ujio wa mfumo utakuwa na manufaa mengi pamoja na uwazi zaidi ambapo hata wanakikundi wenyewe wataweza kuingia na kuona taarifa zao mbalimbali za kifedha popote walipo.

Wanakikundi na wataalam wataweza kuona mwenendo mzima wa shughuli za ukopaji na urejeshaji sambamba na utambuzi wa wahusika wanaohitaji mikopo kwa vigezo vyao kwa kuwa umeunganishwa na mfumo wa taifa NIDA. Kama mkopo ni kwa vijana basi uwe kijana kweli usizidi miaka 35 kwani ukiingiza taarifa zisizo sahihi mfumo hautokuruhusu.



VITABU 240 VYA MUONGOZO WA ELIMU NGAZI YA MSINGI NA SEKONDARI VYAZINDULIWA RASMI ILEMELA



Vitabu 240 vya muongozo wa elimu ngazi ya msingi na sekondari vilizinduliwa na kutolewa kwa walimu wakuu na wakuu wa shule za Msingi na Sekondari za Manispaa ya Ilemela.

Akizindua vitabu hivyo, Ndugu Saidi Kitinga ambae alimwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Ilemela alisema kuwa lengo kubwa la miongozo hii ni kuzitatua changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta ya elimu ambazo Wizara ya Elimu imezibainisha.

“Wizara ya Elimu imeziona changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta ya elimu na kutoa vitabu vya miongozo hii ya mkakati wa kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji ngazi ya elimu msingi na changamoto katika uboreshaji elimu msingi na sekondari kama zana ya kupambana na changamoto hizo”. Amesema Said Kitinga

Ndugu Kitinga aliongeza kusema kuwa miongozo hii inaenda kurahisisha utendaji wa walimu katika shughuli za ufundishaji jambo ambalo litapelekea kuwa na mwelekeo mzuri kielimu lakini pia itafungua njia katika kupambana na umaskini ambao ni moja kati ya maadui wa maendeleo.

Pamoja na hayo aliwapongeza walimu na uongozi mzima wa Manispaa ya Ilemela kwa kazi nzuri ya maboresho ya kitaaluma inayoendelea huku akisisitiza kusimamia vizuri malengo yaliyowekwa ili kuweza kupata matokeo bora.

Nae Afisa Elimu Sekondari, Ndugu Sylvester Murimi amebainisha kuwa miongozo hiyo itatolewa kwa shule zote za Msingi na Sekondari ndani ya Manispaa ya Ilemela ili kuweka usawa katika utendaji na kuongeza ushindani kitaaluma.

“Miongozo hiyo itawafanya walimu kujiimarisha zaidi katika program zilizopo na zilizoongezwa nchi nzima bara na visiwani”, Jamila Khalfan Afisa Taaluma Msingi



UZINDUZI RASMI WA STENDI YA MABASI NA MAEGESHO YA MALORI NYAMHONGOLO



Stendi mpya ya mabasi na maegesho ya malori Nyamhongolo ilizinduliwa rasmi mnamo tarehe 13 Septemba 2022 na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuitaka Ilemela kuwa mfano mzuri wa kuigwa wa ukusanyaji wa mapato katika stendi hii.

Mhe. Dkt Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliutaka uongozi

wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kuhakikisha inasimamia suala zima la ukusanyaji wa mapato katika stendi ya mabasi na eneo la maegesho ya malori Nyamhongolo kwa kuweka mifumo bora ya kielektroniki ya ukusanyaji mapato.

"Nataka Ilemela muwe ni mfano wa kuigwa wa kukusanya mapato katika kituo hiki, hakikisheni mnasimamia na kuweka mifumo bora ya kielektroniki ya ukusanyaji mapatio yanayotokana na kituo hiki, nisingependa kuona mapato yanapotea hivyo mianya yote ya upotevu wa mapato izibwe kabisa".Amesisitiza

Pamoja na hayo alihimiza kuwa anataka kuona mabadiliko katika suala zima la mapato ya Ilemela kufuatia ujenzi wa kituo hiki kwani kituo hiki ni fursa kubwa hivyo anatarajia kuona makusanyo yanaongezeka mara dufu na kuelekeza ufanyike usimamizi mzuri wa kituo.

Aidha aliwataka wananchi kuchangamkia fursa za biashara na ajira zilizopo katika kituo hiki pamoja na kuhakikisha kuwa wanakitunza na kuendelea kuwa safi ili kiweze kudumu.

ILEMELA YAPOKEA VITABU 23, 496 VYENYE THAMANI YA TSH. MILIONI 47.8



Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela imepokea jumla ya vitabu vya kiada 23, 496 vyenye thamani ya Tsh Milioni 47.8 kwa ajili ya shule za msingi na sekondari kutoka serikali kuu kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania (TET).

Kupokelewa kwa vitabu hivi kunaenda kuboresha mazingira ya kujifunza na kujifunzia pamoja na kuinua taaluma, kujengea wanafunzi uwezo wa kitaaluma ujuzi na maarifa hali inayopelekea kufikia uwiano wa kitabu kimoja kwa wanafunzi watatu (1:3) kwa shule za msingi na wastani wa uwiano wa kitabu kimoja

kwa wanafunzi wawili (1:2) kwa shule za sekondari ambapo lengo kuu la serikali ni kufikia uwiano wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi mmoja (1:1).

Kati ya vitabu hivyo vilivyopokelewa, vitabu 5786 vyenye thamani ya Tsh. Milioni 6.56 ni kwa ajili ya shule za msingi ni, vitabu 15249 vyenye thamani ya Tsh. Milioni 33.6 kwa shule za sekondari kwa ajili ya kidato cha kwanza hadi cha tatu, na vitabu 2461 kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha tano na sita vya thamani ya Tsh milioni 7.7

KAMPENI YA UKUSANYAJI DAMU KITAIFA



Mnamo tarehe 26 hadi 30 mwezi Septemba timu ya wataalamu wa sekta ya afya iliweka kambi katika stendi ya mabasi ya Nyamhongolo kwa siku 5 kwa ajili ya zoezi la ukusanyaji wa damu ikiwa ni kampoeni ya kitaifa ambayo iliendeshwa chini ya kauli mbiu, "DAMU HUJENGA UNDUGU TUJITOKEZE KWA WINGI"

Lengo kwa manispaa ya Ilemela ilikuwa ni kukusanya damu kiasi cha Unit 200 hata hivyo hadi zoezi linakamilika zilikuwa zimekusanywa Unit 205 hivyo kuvuka lengo la asilimia 100.

MAPOKEZI YA FEDHA TSHS. BILIONI 2.2 KWA AJILI YA UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA KWA SHULE ZA SEKONDARI

Halmashauri imepokea fedha kiasi cha Tshs. 2,200,000,000.00 (Shilingi bilioni mbili na milioni mia mbili za kitanzania) kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 110 katika shule za sekondari kwa ajili ya maandalizi ya mapokezi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza kwa mwaka 2023.

MATUKIO KATIKA PICHA



Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akikata utepe ikiwa ni ishara ya uzinduzi wa stendi ya mabasi na maegesho ya malori Nyamhongolo Tarehe 13/09/2022



Wananchi katika stendi ya mabasi ya Nyamhongolo walipokuwa wakimsikiliza Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe/ Dkt Philip Isdor Mpango siku ya tarehe 13 Septemba 2022



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe Abdallah Ulega wakilisha samaki katika moja ya vizimba vya ufugaji samaki katika mradi wa vijana Ilemela



Mafunzo ya serikali mtandao yakitolewa na mkufunzi kwa wakuu wa idara na vitengo katika Manispaa ya Ilemela



Vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye Ulemavu wakipatiwa mafunzo ya matumizi ya mfumo mpya wa kielektorniki kwa ajili ya mikopo ya asilimia 10 ya halmashauri



Katikati ni Mstahiki Meya wa Manispaa ya Ilemela Mhe Renus Mulunga pamoja na Naibu Meya wa Manispaa ya Ilemela (Aliyevaa kofia) Mhe. Manusura na Mkurugenzi wa Ilemela Mhandisi Modest Apolinary wakiongoza Baraza la Madiwani la Halmashauri



Wananchi wa Ilemela Kata ya Shibula wakishiriki kampeni ya ujenzi wa vyumba vya madarasa Ilemela



Timu ya Wataalam kutoka Hazina ilipofika kujitambulisha kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela lengo ikiwa ni kufuatilia utekelezaji wa ujenzi wa jengo la utawala na ukusanyaji wa mapato ya ndani

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO



Tsh Milioni 40 za mapato ya ndani ya Halmashauri zimetumika kukamilisha ujenzi wa jengo la kujifungulia katika Zahanati ya Nyakato ujenzi ulianzishwa kwa nguvu za wananchi na fedha za mfuko wa Jimbo



Tsh Milioni 40 za mapato ya ndani ya Halmashauri zimetumika kukamilisha ujenzi wa jengo la kujifungulia katika Zahanati ya Illemela ujenzi ulianzishwa kwa nguvu za wananchi na fedha za mfuko wa Jimbo



ZAHANATI YA LUMALA: Tsh Milioni 151.41 zimetumika kukamilisha ujenzi katika ya fedha hizo Milioni 100 ni fedha kutoka Serikali Kuu, Milioni 5 fedha za Halmashauri na Tshs Milioni 47.2 ni michango ya wananchi na fedha za mfuko wa Jimbo



KITUO CHA AFYA KAYENZE: Kituo hiki kimejengwa kwa fedha za tozo ya miamala ya simu, kiasi cha Tsh Milioni 500 zimepokelewa na kujenga majengo ya; wagonjwa wa nje, maabara, kichomea taka, jengo la kufulia, wodi ya wazazi na upasuaji.



KICHOMEA TAKA: Ujenzi wa kichomea Taka cha kisasa katika hospitali ya Wilaya hadi sasa Jumla ya Tsh Bilioni 3.1 zimepokelewa kwa awamu tatu tofauti kutoka Serikali kuu na jumla ya majengo 14 yameshajengwa



JENGO LA KUHIFADHIA MAITI: Ujenzi wa jengo la kuhifadhia maiti katika hospitali ya Wilaya hadi sasa Jumla ya Tsh Bilioni 3.1 zimepokelewa kwa awamu tatu tofauti kutoka Serikali kuu na jumla ya majengo 14 yameshajengwa

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO



JENGO LA UPASUAJILI: Ujenzi wa jengo la upasuaji katika hospitali ya Wilaya hadi sasa Jumla ya Tsh Bilioni 3.1 zimepokelewa kwa awamu tatu tofauti kutoka Serikali kuu na jumla ya majengo 14 yameshajengwa



HOSPITALI YA WILAYA : Muonekano wa hospitali ya Wilaya hadi sasa Jumla ya Tsh Bilioni 3.1 zimepokelewa kwa awamu tatu tofauti kutoka Serikali kuu na jumla ya majengo 14 yameshajengwa majengo 11 yamekamilika na baadhi ya huduma zinaendelea



BWENI LA WAVULANA: Bweni jipya la wavulana katika shule ya Sekondari ya wavulana ya Bwiru, limekamilishwa kwa kiasi cha Tsh Milioni 71.81 fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri ukamilishaji huu ni pamoja na kuweka vitanda na magodoro



KIWANDA KIDOGO CHA UFYATUJAJI WA MATOFALI: Mradi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ulioanzishwa kupitia chanzo cha mapato ya ndani ya Halmashauri Hadi sasa kiasi cha Tshs. Milioni 226.95 zimetumika kuwezesha shughuli za mradi



SHULE YA SEKONDARI LUMALA: Jumla ya madarasa 6 yamejengwa kupitia fedha za UVIKO-19 kutoka serikali kuu Gharama ya ujenzi wa madarasa haya ni Tshs. Milioni 120 kila darasa lilijengwa kwa Tshs. Milioni 20. Manispaa ya Ilemela ilipokea fedha kiasi cha Tshs. Bilioni 1.94 kwa ajili ya madarasa 97



ANWANI ZA MAKAZI: uwekaji wa anwani za makazi, Jumla ya Tsh Milioni 236.46 zimetumika kutekeleza mradi huu, ambapo fedha kiasi cha Tshs. Milioni 132.38 ni fedha kutoka serikali kuu, Milioni 74.27 fedha za Halmashauri, Tshs Milioni 14.9 fedha za TARURA na wananchi wamechangia Tshs. Milioni 14.85


UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO



MADAWATI ELIMU MSINGI: Utengenezaji wa madawati kwa ajili ya shule za msingi kupitia mapato ya ndani ambapo Halmashauri imetoa kiasi cha Tsh Milioni 35 kutoka chanzo cha mapato ya ndani ya Halmashauri na jumla ya madawati 500 yametengenezwa



UKARABATI WA MIUNDOBINU YA MASOKO: Tshs. milioni 84 za mapato ya ndani ya Halmashauri zimetumika kukarabati miundombinu ya masoko ya Halmashauri imehusisha pia ukarabati wa vyoo katika masoko hayo.



UJENZI WA MFUMO WA MAJI MASHULENI: Kiasi cha Tsh Milioni 35.30 fedha kutoka WASH zimetumika kujenga miundombinu ya usafi wa kunawa mikono kwa wanafunzi wa shule za Msingi za Buswelu na Tumaini na Shule ya Sekondari nyamanoro



UJENZI WA MATUNDU YA VYOO: Ujenzi wa matundu ya vyoo kwa fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri katika shule za Sekondari na Msingi. Shule ya Sekondari Lumala yamejengwa matundu 12, Sekondari ya Masanza matundu 12, Sekondari ya Ilogwe matundu 12 Semba B matundu 10, Sekondari ya Nyamhongolo matundu 12, na matundu 9 ya vyoo katika shule mpya ya msingi ya Bujingwa



OFISI YA MTA: Ukamilishaji wa ujenzi wa ofisi za mtaa na ofisi za Kata katika manispaa ya Ilemela; Ofisi mbili za mtaa wa Kayenze na Nyambiti zimekamilishwa kwa gharama ya Tshs. Milioni 12.58 na ukamilishaji wa ofisi ya Kata ya Bugogwa kwa Tshs. Milioni 15 fedha za mapato ya ndani



SHULE YA SEKONDARI SEMBA B: Fedha kiasi cha Tshs. Milioni 57.33 za mapato ya ndani zimetumika katika ukamilishaji wa madarasa 7, ujenzi wa matundu 10 ya vyoo na ofisi moja ndogo shule mpya ya sekondari Semba B kata ya Shibula.

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO



SHULE YA SEKONDARI MASANZA: Fedha kiasi cha Tshs. Milioni 77.83 za mapato ya ndani zimetumika kwa ajili ya Ukamilishaji wa madarasa 4, maabara 2, matundu 12 ya vyoo na ofisi moja ndogo shule mpya ya sekondari Masanza Kata ya kahama na Tshs Milioni 10.4 zimetumika kutengeneza meza na viti 200



UNUNUZI WA MAGARI: Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kupitia makusanyo yake ya ndani imeweza kununua magari 4 kwa ajili ya shughuli za mapato na ufuatiliaji wa miradi kwa gharama ya Tshs. Milioni 532.2 magari 2 yamepokelewa



SHULE YA SEKONDARI NYAMHONGOLO: Kiasi cha Tsh Milioni 30 fedha za mapato ya ndani zimetumika kwa ajili ya ukamilishaji wa madarasa 2, matundu ya vyoo 12 na ofisi ndogo 1 shule ya sekondari Nyamhongo



BARABARA YA BREWERIES: Ujenzi wa barabara hii ni ya kiwango cha lami nyepesi yenye urefu wa kilomita 0.9kalvati pamoja na mtaro mita 1000 kwa gharama ta Tshs. Milioni 499.95 Fedha za tozo za mafuta, barabara imesimamiwa na TARURA



NYUMBA YA WALIMU: Tshs Milioni 20 za mapato ya ndni ya Halmashauri zimetumika kukamilisha nyumba ya walimu (2 in 1) katika shule ya msingi CHASUBI



SHULE YA SEKONDARI BUZURUGA: Hii ni shule mpya katika kata ya Buzuruga inayojengwa kupitia fedha mpango wa maendeleo ya elimu sekondari (SEQUIP) majengo 14 na matundu 20 ya vyoo yamejengwa. Fedha kiasi cha Tshs. Milionu 470 zimepokelewa kutoka serikali Kuu

HALIUZWI






Jarida hili Limehaririwa na Kusanifiwa na:
Violancea Mbakile
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela

Waandishi na Wapiga Picha Wasaidizi:
Paschalia George na Yusuph Ludimo

SCAN HAPA KUPERUZI
TOVUTI YA ILEMELA



OFISI YA MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA
200BR.YA BUSWELU
33282 BUSWELU
ILEMELA,MWANZA

Tufuatilie >>>      **ilemelamamc |  www.ilemelamc.go.tz**
Barua Pepe: md@ilemelamc.go.tz